



Miongo Mitano ya Fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania: Maendeleo, Changamoto na Mustakabali Wake

Alex Umbima Kevogo

Idara ya Lugha, Isimu na Fasihi,
St Agostino University, Tanzania
umbima2000@gmail.com

Tanzania inaposherehekea miaka hamsini ya uhuru, makala haya yamechunguza historia na maendeleo ya fasihi andishi ya Kiswahili ya Tanzania ndani ya kipindi cha miongo mitano baada ya uhuru. Msisitizo maalumu umekitwa kwenye mikondo ifuatayo inayojitokeza: (a) Kuibuka kwa fasihi inayoihakiki jamii (b) Kuibuka kwa fasihi ya kimajaribio (c) Chimbuko la fasihi pendwa (d) Kuzuka kwa fasihi ya kizalendo (e) Athari za utandawazi na tafsiri za kazi za fasihi zenye asili ya kigeni. Haya yote yamezingatia mkabala wa kihistoria unaotathmini maendeleo ya kijamii, kisiasa, kitamaduni na kiuchumi nchini Tanzania miaka hamsini baada ya uhuru.

Utangulizi 1.0

Miongoni mwa lugha za Kiafrika, Kiswahili ndiyo lugha ya pekee iliyo na wazungumzaji wengi barani Afrika. Takribani wazungumzaji milioni 70 huitumia lugha hii katika mataifa ya Afrika ya Kati na Mashariki. Baadhi ya mataifa hayo ni Tanzania, Kenya, Burundi, Rwanda, Visiwa vya Komoro, Uganda, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, Madagascar, Mozambique, Zambia na Sudan Kusini. Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Tanzania, Kenya na Uganda. Istilahi fasihi ya Kiswahili Tanzania imetumiwa kwenye muktadha unanaoifasili kuwa fasihi iliyotungwa katika lugha ya Kiswahili nchini Tanzania.

Fasihi andishi ya Kiswahili ilianza kupata ufanisi Afrika Mashariki baada ya 1970 kutokana na mazingira ya kisiasa ya kipindi hicho. Kabla ya hapo, kazi za fasihi zilizotungwa ni zile zilizofadhiliwa na wakoloni kati ya 1930 hadi 1950. Nchini Tanzania, mshairi mzalendo *Shabaan Robert* (1909-1962) alitunga mashairi na riwaya za kizalendo baina ya 1952-1957. Shabaan Robert alitunga jumla ya Diwani za ushairi kumi na tatu. Diwani hizo ni hizi zifuatazo: *Almasi za Afrika* (1972), *Koja la Lugha* (1969), *Insha na Mashairi, Kielelezo cha Fasili* (1968), *Pambo la Lugha* (1966), *Ashiki Kitabu Hiki* (1968), *Mashairi ya Shabaan Robert* (1968), *Sanaa ya Ushairi, Mwafrika Aimba* (1946), *Masomo yenye Adili, Tenzi na Marudi Mema na Omar Khayyan, Utenzi wa Vita vya Uhuru na Mapenzi Bora*. Shabaan Robert aliandika jumla ya kazi za nathari nane ambazo ni hizi zifuatazo: *Maisha Yangu na Baada ya Miaka Hamsini* (1966), *Kusadikika* (1951), *Adili na Nduguze* (1952), *Kufikirika* (1951), *Kielelezo cha Insha, Wasifu wa Siti Binti Saad, Utubora Mkulima* (1968) na *Siku ya Watenzi Wote* (1968). Kwenye visiwa vya Zanzibar, riwaya za upelelezi za *Muhammed Said Abdulla* zilianza kujitokeza kwenye kipindi hicho.

Mataifa mengi Afrika yanayotumia lugha ya Kiswahili katika mawasiliano yalipata uhuru miaka ya mwanzo ya 1960. Uchumi wa mataifa haya uliendelea kunawiri kutokana na uongozi bora, amani na ari au msukumo wa kizalendo wa raia na viongozi walioshika hatamu za uongozi. Hata hivyo, hali hii haikudumu kipindi kirefu kwa sababu kuanzia mwaka wa 1973 tatizo la uhaba wa mafuta na bei za juu za nishati ziliathiri uchumi wa mataifa haya. Matokeo yake yalikuwa mfumko wa uchumi uliosababisha ugumu wa maisha miongoni mwa raia uliosababisha migogoro ya kijamii na uasi uliokithiri. Hali hii iliwachochea wasanii mbalimbali kutathmini upya imani, itikadi, sera na nguzo za kitaifa zilizokuwa zimepuuzwa awali. Enzi hii ilishuhudia kuibuka kwa kizazi kipya cha wasanii waliojihami kwa ari mpya, mwamko mpya na urazini mpya wa kisiasa. Wasanii hawa walijihami kwa silaha mpya ya kazi za fasihi zenye muundo, umbo na mwelekeo mpya uliokiuka kaida zilizozoeleka. Silaha hii ilifanikiwa kubomoa nguzo na misingi ya ngome ya fasihi ya Kiswahili ya kimapokeo.

Lengo kuu la utafiti huu ni kuchunguza historia na maendeleo ya fasihi ya Kiswahili ya Tanzania ndani ya kipindi cha miongo mitano baada ya uhuru na athari za msukumo wa nguvu za kiuchumi, kijamii, kisiasa, kitamaduni na kiutandawazi. Makala haya yanahoji kwamba kuna mikondo mitano inayobainisha hatua za maendeleo zilizopigwa kwenye fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania miaka hamsini baada ya uhuru.

2.0 Usuli Wa Mada

Kimsingi fasihi ya Kiswahili ingali katika hali ya kutegemea usimulizi. Ubunifu simulizi hutokea katika shughuli mbalimbali za jamii kwa mfano ngo-ma, arusi, kazi, jando, unyago, matibabu, matambiko na ibada. Hata hivyo, uchunguzi wa aina hii ya fasihi ni mpana zaidi na hauwezi kuzingatiwa kwenye makala kama hii. Fasihi andishi ya Kiswahili japo ni changa na banifu ikilinganishwa na fasihi simulizi ina historia ya zaidi ya miaka 500. Inakisiwa kwamba fasihi andishi ya Kiswahili ilianza kwenye upwa wa Afika Mashariki baada ya kuanzishwa kwa hati za Kiarabu. Dai hili haliwezi kuthibitishwa kutokana na ukosefu wa ushahidi kamili au stakabadhi zilizoandikwa wakati huo. Ithibati kamili ya kazi ya kwanza ya fasihi andishi ya Kiswahili ni *Siri l'Asirari* iliyotungwa na *Binti Bwana Lemba* mwaka wa 1663.

Utanzu wa awali zaidi katika fasihi andishi ya Kiswahili ni ushairi. Utanzu huu ulipata kunawiri katika karne ya 18 na 19. Baadhi ya kazi maarufu zilizotungwa kipindi hiki ni *Utendi wa Tambuka* uliotungwa na *Bwana Mwengo Bin Athumani* (1728), *Utenzi wa Hamziyya* uliotungwa na *Said Aidarus* (1749), *Utenzi wa Al-Inkishafi* uliotungwa na *Said Abdullah Bin Nasir* (1800) na *Utenzi wa Ras l Ghuli* uliotungwa na *Mgeni Bin Faqini* (1855). Kazi hizi zilichochewa na dini ya Kiislamu. Hata hivyo, maudhui yake ni mapana kiasi kwamba yanahusisha falsafa ya dini na masuala ya ukombozi dhidi ya utawala wa mabavu wa Wareno, Waingereza na Wajerumani Afrika Mashariki.

Kuenea kwa kasi kwa lugha ya Kiswahili Afrika ya Kati na Mashariki katika karne ya 19 kupitia kwa biashara na sera za serikali za ukoloni baada ya 1900, kulisababisha mabadiliko ya fasihi andishi ya Kiswahili ambayo yaliigeuza kutoka kwa hali ya kuwa fasihi ya eneo moja hadi kuwa fasihi ya kitai-fa. Kufikia miaka ya 1940 vitabu viliaanza kuchap-

ishwa katika lugha ya Kiswahili nchini Tanzania. Baadhi ya waandishi maarufu wa kipindi hiki ni *Amri Abeid* (1965) na *Mathias Mnyampala* (1969) ambao hawakuwa Waswahili.

Kuanzishwa rasmi kwa Kamati ya Lugha Afrika Mashariki miaka ya 1930 iliyokabidhiwa jukumu la kusanifisha lugha ya Kiswahili kuliikuza fasihi andishi ya Kiswahili ya Tanzania. Vitabu vingi vya kigeni vilitafsiriwa katika lugha ya Kiswahili. Hata hivyo, uchapishaji halisi haukuanza mara moja, ulikawia hadi mwaka wa 1946 lilipoanzishwa Shirika la Uchapishaji Vitabu la Afrika Mashariki (EALB). Dhima kuu ya Shirika hili ilikuwa kuchapisha vitabu katika lugha za Kiafrika na Kiingereza. Inahalisi kudai kwamba idadi kubwa ya vitabu vilivyochapishwa kuanzia miaka ya 1920 hadi 1940 vilikuwa vitabu vya shule.

Migogoro ya kizalendo nchini Tanzania iliyoongozwa na wafanyakazi pamoja na wazalendo dhidi ya utawala wa dhuluma wa wakoloni miaka ya 1920 hadi 1950 iliunganishwa na lugha ya Kiswahili. Baada ya uhuru lugha ya Kiswahili ilipata dhima mpya ikawa lugha ya taifa. Lugha ya Kiswahili ilipopata hadhi kuu, hitaji la kuitumia kuandaa kazi za fasihi liliongezeka. Azimio la Arusha la mwaka wa 1967 lililoibadishi rasmi sera ya uongozi nchini Tanzania kuwa Ujamaa lilisababisha kuongezeka kwa elimu ya watu wazima na kupanua elimu ya shule za msingi. Hali hii ilisaidia sana kuendeleza lugha ya Kiswahili pamoja na fasihi yake nchini Tanzania. Baada ya mwaka wa 1970 utulivu ulioshuhudiwa nchini Tanzania ulisaidia kuandaa mazingira endelevu yaliyosababisha kunawiri kwa fasihi andishi.

3.0 Mikondo Mikuu ya Maendeleo katika Fasihi ya Kiswahili nchini Tanzania: 1961-2011

Uhakiki wa kina wa fasihi andishi ya Tanzania baada ya uhuru unabainisha mikondo mitano ya maendeleo ya fasihi hiyo. Tutaijadili kwa kina mikondo hiyo tukitumia kazi mbalimbali za fasihi

zilizotungwa baada ya uhuru huku tukionyesha hatua za maendeleo zilizopigwa kuanzia wakati huo hadi kufikia sasa.

3.1 Kuibuka kwa Fasihi inayoihakiki Jamii

Fasihi inayoihakiki jamii haikuanza nchini Tanzania baada ya uhuru. Fasihi ya aina hii ilikuwapo Tanzania kabla ya uhuru wakati ambapo waandishi kama vile *Amri Abeid*, *Saadani Kandoro* na *Shaaban Robert* walitunga kazi za kitashtiti kushambulia utawala wa kikoloni. Baadhi ya Kazi hizi ni riwaya za mwanzo za Shaaban Robert kwa mfano *Kusadikika* (1951), *Adili na Nduguze* (1951) na *Kufikirika* (1957) ambazo zilikashifu ukoloni japo kwa kutumia mbazi, taashira na jazanda za kiistiari. Hata hivyo, ni baada ya uhuru ndipo fasihi iliyoihakiki jamii kwa uhalisia wake ilipoanza kuenea na kusambaa.

Fasihi ya uhakiki wa kijamaa iliibuka baada ya uhuru kama witikio wa itikadi ya kisoshalisti iliyopendekezwa kwenye Azimio la Arusha na utekelezaji wake. Azimio lilizaliwa mwaka 1967 kwa madhumuni ya kuwa mwongozo wa ufafanuzi na utekelezaji wa itikadi na sera za Tanzania ambayo wakati huo ilikuwa imeamua siasa ya kijamaa. Aina hii ya fasihi ilianza baada ya kuchapishwa kwa tamthiliya ya kihistoria ya *Ebrahim Hussein* ijulikanayo kama *Kinjeketile* (1969). Tamthiliya hii inasawiri tukio la kihistoria linalohusu mapambano ya Watanzania dhidi ya nguvu za mkoloni. Mwandishi ametumia sitiari kuangaza manufaa na upungufu wa ujamaa kama mfumo wa Kiafrika unaomuunganisha mwafrika kwenye msako wa uhuru wa kudumu. Tamthiliya hii ilifuatiwa na *Mashetani* (1971), *Ngao ya Jaji* (1976) na *Jogoo Kijijini* (1976). Tamthiliya hizi zinadadisi kwa kina na kuihakiki jamii kwa jicho pevu ili kuuelewa ukweli kuhusu suala la maana ya uhuru, dhuluma, uhasama, mivutano ya kitabaka na mitanziko ya kisaikolojia iliyosababishwa na kupitishwa kwa Azimio la Arusha. Tamthiliya hizi ni vielelezo vya utungaji wa tamthiliya wa hali ya juu na ndiyo sababu ya mwandishi wake kutunukiwa tuzo ya mwandishi bora wa tamthiliya na Muungano wa Waandishi wa Afrika mwaka wa 1988.

Mwandishi mwingine shupavu wa fasihi ya uhakiki wa kijamaa ni Kezilahabi Euphrase. Riwaya yake ya kwanza ni *Rosa Mistika* (1970). Riwaya hii ilifuatwa na Diwani ya *Kichomi* (1973), *Kichwamaji* (1974), *Dunia Uwanja wa Fujo* (1975), *Gamba la Nyoka* (1979), *Nagona* (1987), *Karibu Ndani* (1989), *Mzingile* (1993), *Kaptula la Marx* (1996) na *Dhifa* (2008). Baadhi ya Hadithi Fupi alizozitunga ni

Mayai Waziri wa Maradhi (1992), *Magwanda Kubilya na Vyama Vingi* (1992). *Cha Mnyonge Utakitapika Hadharani* (1992) na *Wasubiri Kifo* (1992). Hadithi hizi zinatumia upanga wa tashtiti kukata kitanzi cha uozo kinachotishia kuiangamiza jamii.

Kezilahabi ni mkakiki wa jamii anayejiuliza maswali kuhusu kila kipengele cha maisha kuanzia miundo ya jamii ya kitamaduni, dini, elimu ya kimagharibi, siasa hadi falsafa. Isitoshe Kezilahabi ni mwazaji anayeihakiki kila sehemu ya maisha ya jamii kwa uhalisi unaoshangaza. Mwandishi huyu ni bingwa anayesawiri dhamira zake akizingatia mkabala wa kidhanaishi unaoweka wazi kero na mitanziko ya wanyonge katika jamii yake. Mhusika wake maarufu ni mkinzani wa mbabe ambaye mara nyingi ni msomi wa tabaka la kati anayejikuta kwenye njia panda. Mhusika huyu anakumbwa na hali mbili zinazomtatiza: ajiamini binafsi na kufuata mkondo wake binafsi wa fikra au afuate jamii inayomtegemea atoe uongozi na kuibadilisha. Hatamiye hulemewa na mzigo wa kufanya uamuzi wa busara kisha hukimbilia kuyamaliza maisha yake anapojiua. Mhusika huyu haoni maana ya maisha, amekengeuka na kukata tamaa.

Mwandishi mwingine mashuhuri anayeihakiki jamii yake baada ya kupitishwa kwa Azimio la Arusha ni *Penina Muhandu Mlama*. Mwandishi huyu wa tamthiliya anakashifu viongozi wanaowasaliti wananchi kwa kuyakubali masharti yanayowekwa na Mashirika ya Ufadhili kama vile IMF na Benki Kuu ya Dunia. Baadhi ya dhamira anazozizingatia ni migogoro ya kiutamaduni, migogoro kuhusu maadili kwenye jamii za jadi na vijiji vipya vya ujamaa, ukengeushi wa wasomi, usawa wa kijinsia na taathira za tamaa na ubinafsi katika jamii. Baadhi ya tamthiliya maarufu alizozitunga ni *Hatia* (1972), *Tambueni Haki Zetu* (1973), *Pambo* (1975), *Nguzo Mama* (1982), *Lina Ubani* (1984) na *Wizara ya Mitumba* (?)

Swala la uozo wa kijamii zimewashughulisha waandishi wengi nchini Tanzania kwa nia ya kujenga jamii mpya adilifu. Mwandishi maarufu anayelitalii swala hili ni Chachage C. S. aliyandika riwaya zifuatazo: *Kivuli* (1981), *Sudi ya Yohana* (1981), *Almasi za Bandia* (1990) na *Makuadi wa Soko Huria* (2005). Baadhi ya waandishi wamesimulia ukweli kupitia kwa ucheshi. Miongoni mwao ni C. Mung'ong'o mwandishi wa riwaya za tashtiti kama vile: *Njozi Iliyopetea* (1980) na *Mirathi*

ya *Hatari* (1977). Wa pili ni Gabriel Ruhumbika mwandishi wa Hadithi Fupi za tashtiti kwa mfano: *Wali wa Ndevu na Hadithi Nyingine* (1974), *Parapanda* (1974) na *Uwike Usiwike Kutakucha* (1978). Mwandishi huyu anashambulia ufisadi, unfiki, uzandiki na uozo mwingine kwa upanga wa tashtiti. Mwandishi wa mwisho ni Harisson Mwakyembe aliyeandika riwaya ya tashtiti ijulikanayo kama *Pepo ya Mabwege* (1974). Wengine kwenye mkondo huu ni Liwenga G Nyota ya *Huzuni* (1974); Saffari J. Abdallah, *Kabwela* (1978) na *Harusi* (1984) na Martha Mvungi, *Lwidiko* (1979). Waandishi hawa wanasaili masaibu yaliyopoteza mwelekeo kuenenda kwenye nchi ya ahadi iliyoahidiwa na sera ya ujamaa.

Kuna waandishi wanaohakiki shughuli za kilimo katika jamii baada ya kupitishwa kwa Azimio la Arusha. Suala kuu wanalolishughulikia ni iwapo sera ya Ujamaa vijijini ilifaulu kumkomboa mkulima au ni chombo cha ukandamizaji kilichotumiwa na wachache wenye ubinafsi wakitumiwa na mataifa ya Kimagharibi kumdhulumu mkulima. Miongoni mwao ni C. Chachage, *Kivuli* (1981), N. Nghalyoma, *Kijiji Chetu* (1975), E. Kezilahabi, *Gamba la Nyoka* (1979) na K. Kahigi na A. Nge-mera, *Mwanzo wa Tufani* (1976)

Mwelekeo mpya kwenye mkondo huu wa fasihi ni ule wa fasihi inayomlenga mnyonge katika jamii. Mkondo huu ulizuka kipindi cha baada ya 1979 ambapo Tanzania ilitoswa katika hali ngumu kiu-chumi. Hali hii iliendelea hadi mwaka 1984 ambapo sera ya soko huria ilianzishwa. Aina hii ya fasihi ilizuka miaka ya 1980 na kuendelea, lengo lake kuu ni kuyaweka wazi madhila ya wanyonge na kero zao katika jamii. Mwandishi maarufu anayezingatia mkondo huu ni Said Ahmed Mohamed aliyetunga kazi zifuatazo: *Dunia Mti Mkavu* (1980), *Utengano* (1980), *Sikate Tamaa* (1981), *Kina cha Maisha* (1988), *Kiza Katika Nuru* (1988), *Asali Chungu* (1989), *Tata za Asumini* (1990), *Amezidi* (1995), *Kitumbua Kimeingia Mchanga* (2000), *Babu Alipofufuka* (2001), *Sadiki kipenda na Hadithi Nyingine* (2002), *Arusi ya Buldoza na Hadithi Nyingine* (2005), *Mfuko Mtupu na Hadithi Nyingine* (2005), *Dunia Yao* (2006), *Siku ya Siku na Hadithi Nyingine* (2008) na *Nyuso za Mwanamke* (2010). Mwingine ni Adam Shafi aliyeandika riwaya zifuatazo: *Kasri ya Mwinyi Fuadi* (1978), *Kuli* (1979) *Vuta n'Kuvute* (1999) na *Haini* (2003).

Ni bayana kwamba fasihi andishi ya Kiswahili ya

wakati huu ilitumiwa kama mwenge wa kuangaza hali kamili ya mwananchi wa kawaida katika hali na eneo lolote lile la kijamii na kuonesha matarajio yake, matamano yake na kero zake za kila siku. Fasihi hii ni kipaza sauti cha mwananchi anachokitumia kudai haki zake za kimsingi na pia kukashifu uozo katika jamii yake.

3.2 Fasihi ya Kizalendo

Mkondo huu wa fasihi ulizuka baada ya uhuru ukafikia kilele miaka ya 1970 na 1980. Dhamira kuu ya aina hii ya fasihi ilikuwa kumuasa mwafrika kujivunia hali yake ya Uafrika, kuuthamini utamaduni wake na kukashifu uigaji wa tamaduni na mitindo ya kigeni. Baadhi ya waandishi walikuwa mstari wa mbele kumwelimisha mwanajamii ili kumkomboa kimawazo. Mfano ni J. K. Kiimbila, *Ubeberu Utashindwa* (1971), F. Senkoro, *Mzalendo* (1978), M. Mulokozi, *Mkwawa wa Uhehe* (1979), E. Mbogo *Tone la Mwisho* (1981) na P. Muhando, *Harakati za Ukombozi* (1982). Kazi hizi zinalenga kumwelimisha Mtanzania kuhusu maana kamili ya uhuru katika mazingira ya baada ya utawala wa mkoloni.

Fasihi ya kizalendo inayousifia utamaduni wa Mwafrika ilichipuka baada ya riwaya ya S. Farsy, *Kurwa na Doto* (1960) kutungwa. Riwaya hii ilifutwa na ile ya F. Nkwera, *Mzishi wa Baba ana Radhi* (1967) na kufikia kilele mwaka wa 1982 baada ya kuchapishwa kwa riwaya ya A. Kitereza, *Bwana Myombekere na Bibi Bugonoka na Ntulanalwo na Bulihwali*. Riwaya hii inasifika kwa usawiri wake halisi wa maisha na utamaduni wa Mwafrika kabla ya ukoloni.

Kuna baadhi ya waandishi waliouona ujamaa katika jicho la namna wahenga wetu walivyoishi pamoja; kwa hiyo walipendekeza jamii yetu irejee misingi ya jadi ya Mwafrika inayoendelea kutoweka. Kundi hili liliandika kazi zao kwa kusawiri maisha yaliyopita. Mfano wa aina hii ya fasihi ni riwaya ya George Mhina, *Mtu ni Utu* (1971) na ile ya Seme W, *Njozi za Usiku* (1972) zinazoshadidia mfumo wa maisha ya wahenga kwa kusisitiza ushirikiano. Waandishi wengine waliuona ujamaa kwa jicho la matarajio kwamba kuna ujenzi wa jamii mpya itakayoishi vyema kuliko hii ya sasa. Watunzi wake walikuwa na hamu, maono au shauku ya wakati ujao. Mifano ya aina hii ya fasihi ni riwaya ya Ngomoi J, *Ndoto ya Ndaria* (1975) na *Shida* (1975) iliyoandikwa na Ndyanao Balisidya. Riwaya hizi zili-

hamasisha kuhusu maisha katika vijiji vya ujamaa na kuyaonyesha kuwa bora kuliko yale ya mjini.

Fasihi ya kizalendo inaendelea kudidimbia sio nchini Tanzania pekee bali Afrika Mashariki na kote Afrika pia. Tishio kubwa ni athari za utandawazi zinazowafanya waandishi wapya kuusifia utamaduni wa kigeni.

3.3 Fasihi Pendwa

Fasihi pendwa nchini Tanzania ililenga matabaka mawili ya wasomaji yaani tabaka la kati na lile la chini ambalo lina kiwango cha chini cha elimu. Fasihi pendwa iliyolenga tabaka la kati ina sifa zifuatazo: ina kiwango cha juu cha usanii, wahusika changamani na msuko changamani. Sifa hizi huzifanya kazi za fasihi za tabaka hili kuwa na kurasa nyingi, kwa hiyo gharama yake ni ya juu. Baadhi ya waandishi wanaolenga tabaka hili ni *Ben Mtobwa* na *Eric Shigongo*. Kwa upande mwingine, fasihi pendwa inayolenga tabaka la chini inatumia lugha rahisi iliyo wazi, wahusika bapa na msuko sahili. Vitabu hivi vina gharama nafuu ili vinunuliwe na wasomaji wote kwa mfano vitabu vilivyochapishwa na *Ndanda Mission Press* miaka ya 1970.

Fasihi pendwa nchini Tanzania ilichipuka miaka ya 1960 na kufikia kilele baina ya 1970 na 1990. Aina hii ya fasihi ina kazi zinazozingatia uhalifu, makosa ya jinai na mahaba ambazo zina wahusika wahalifu wanaotabirika wanaotekeleza makosa ya jinai na kusakwa na maafisa wa usalama. Pengine hadithi hizi huwa na mashujaa wa upelelezi wanaowasaka wahalifu hadi wanapowakashika. Aidha kuna mashujaa wa ujasusi wanaotekeleza upelelezi wa kimataifa.

Mwandishi shupavu na mwanzilishi wa aina hii ya fasihi nchini Tanzania ni Muhammed Said Abdulla aliyandika riwaya zifuatazo za upelelezi: *Mzimu wa Watu wa Kale* (1960), *Kisima cha Giningi* (1968), *Duniani Kuna Watu* (1973), *Siri ya Sifuri* (1974), *Mke Mmoja Waume Watatu* (1975), *Mwana wa Yungi Hulewa* (1976) na *Kosa la Bwana Msa* (1984).

Mwandishi mwingine maarufu wa fasihi ya aina hii ni Ben Mtobwa, *Pesa Zako Zinanuka* (2005), *Dar-es-Salaam Usiku* (2005), *Tutarudi na Roho Zetu* (1987), *Harakati za Joram: Njama ya Pazia* (2004) na *Dimbwi la Damu* (1984). Mwingine ni Simbamwene Simon aliyandika, *Mwisho wa Mapenzi* (1971), *Kweli Unanipenda?* (1978),

Kivumbi Uwanjani (1978), *Madhambi ya Elita* (1982), *Mapenzi ya Pesa* (1984), *Anatafutwa Kuisaidia Polisi* (1984), *Akuanzae Mmalize* (1984), *Madhambi ya Mwenye Nyumba* (1984), *Dogodogo Wanitesa* (1985), *Operesheni Sukuma Namba Nane* (1985), *Chini ya Ulinzi* (1985), *Wa Mwisho Kufa* (1986), *Muuaji ni Nani?* (1987) *Sitaki Kufa* (1987), *Mauaji Lojingi* (1987), *Funguo za Siri Zimeibwa* (1988), *Mume Wangu Asijue* (1988), *Mwamuzi ni Kifo: Mfululizo wa Mume Wangu Asijue* (1988), *Sikutaki Umefilisika* (1988), *Usalama Polisi* (1988), *Orodha ya Watakaouawa* (1988), *Safari ya Hatari* (1989), *Operesheni Msako Kabambe* (1989), *Mlete-ni Nimuue Mwenyewe* (1989), *Nimejitakia* (1989), *Yaliyompata Mpiga Picha* (1990) na *Kwa Sababu ya Pesa* (2007).

Mwandishi mashuhuri wa riwaya pendwa yenye taharuki ni F. Katalambula aliyandika riwaya zifuatazo: *Simu ya Kifo* (1965), *Pili Pilipili* (1977) na *Buriani* (1972). Wengine kwenye mkondo huu ni: Eddie Ganzel, *Faili Maalum* (1978), *Kitanzi*, (1984) na *Kijasho Chembamba*, (1980); A. Musiba, *Njama* (1989), *Zawadi ya Ushindi* (1987), *Hofu* (1997) na *Kikosi cha Kisasi* (1989) na Eric Shigongo, *Rais Anampenda Mke Wangu* (2003) na *Siri Iliyotesa Moyo Wangu*, (2003). Kazi hizi zinashughulikia dhamira za usaliti katika mapenzi, uhalifu, kisasi, mauaji, ukatili na upelelezi. Ujumbe muhimu unaowasilishwa ni kuwa uhalifu haulipi chochote.

Wahakiki mbalimbali wa fasihi andishi kutoka Tanzania wametathmini mchango wa aina hii ya fasihi katika ukuzaji wa maadili na maendeleo ya jamii. Umuhimu wake unabainika upande wa kuwa chombo muhimu cha kuiburudisha jamii na pia ni njia ya kujikimu ya mwandishi na mashirika yanayochapisha vitabu. Hata, hivyo, kuna haja ya kuendeleza aina hii ya fasihi kwa sababu baadhi ya vitabu vilivyoandikwa vimeathiri kuandaliwa kwa filamu almaarufu kwa lakabu ya 'filamu za kibongo.'

3.4 Fasihi ya Kimajaribio

Mkondo wa fasihi ya kimajaribio ulianza miaka ya 1970 hadi miaka ya 1990. Mtindo wa kimajarabio uliathiri umbo, fani na maudhui ya kazi ya fasihi. Kabla ya hapo wasanii wengi walizingatia maumbo, fani na maudhui ya kimapokeo. Hali ilibadilika baada ya Azimio la Arusha. Wasanii wengi walijiona huru na kupata nguvu na ari mpya bila kuthibitwa na kaida za kimapokeo.

Athari ya kwanza ya Azimio la Arusha katika fasihi ya Kiswahili ilishuhudiwa mwaka wa 1968 wakati ambapo mshairi mashuhuri *Mathias Mnyampala* alipoanzisha mashairi ya malumbano yaliyojulikama kama *ngonjera*. Ushairi wa aina hii ulitumiwa kueneza itikadi na sera za Ujamaa. Japo kimsingi ngonjera ni ushairi wa kimapokeo ulio na asili katika jamii za Kiafrika, ulipewa maudhui mapya na mbinu mpya za uwasilishaji kwa hadhira zilizoifanya kuwa sanaa ya utendaji na wala sio ya kusomwa na hadhira.

Kwenye uandishi wa tamthiliya majaribio yalishuhudiwa mara ya kwanza kupitia kwa tamthiliya za Ebrahim Hussein: *Ngao ya Jadi* (1976) na *Ujamaa Vijijini* (1976), Penina Mlama: *Lina Ubani* (1984), M. Mulokozi: *Mkwava wa Uhehe* (1979). Katika tamthiliya hizi za kimajaribio wasanii wanajaribu kubadilisha sanaa za maonesho za jadi kama vile masimulizi ili ziwe za kisasa kama ilivyo katika mataifa ya Kimagharibi.

Mitindo ya kimajaribio ilianza kujitokeza kwenye ushairi wa Kiswahili wa Tanzania kuanzia mwaka wa 1973. Mitindo ya kimajaribio ilianzishwa na washairi chipukizi waliofunzu kutoka Vyuo Vikuu walioanza kutunga mashairi huru. Miongoni mwao ni E. Kezilahabi: *Kichomi* (1974) na *Karibu Ndani* (1988), M. Mulokozi na K. Kahigi: *Malenga wa Bara* (1976), *Mashairi ya Kisasa* (1973) na *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu* (1979), S. A. Mohammed: *Sikate Tamaa* (1980) na *Kina cha Maisha* (1984), T. Mvungi: *Chungu Tamu* (1985), P. Kija: *Wimbo wa Kandambili* (1987), A. Saleh: *Changamka* (1988). Washairi hawa waliasi sheria za kimapokeo zilizoongoza utunzi wa mashairi. Wasanii wakimajaribio walichukulia sheria za utunzi kuwa pingu zilizoufunga ushairi wa Kiswahili utumwani na hazikuweza kukidhi mahitaji ya ushairi wa kisasa.

Upande wa riwaya ya Kiswahili mitindo ya kimajaribio ilianza kushuhudiwa baada ya kuchapishwa kwa riwaya za E. Kezilahabi: *Nagona* (1987) na *Mzingile* (1993) kwenye riwaya hizi mwandishi anatumia mitindo mipya ya usawiri wa wahusika na matukio zinazokiuka mitindo ya riwaya ya jadi iliyozoeleka. Baadhi ya sifa za riwaya hii ni ile ya kushughulikia kwa kina matatizo yanayoikabili dunia ya sasa. Riwaya hii imeshughulikia matatizo ya ndani ya nchi na jamii husika kwa kiwango fulani, lakini kwa kiasi kikubwa imekiuka mipaka ya kitaifa na kieneo na kuangalia hali ya mataifa ya

ulimwengu kwa mfano tatizo la utandawazi. Riwaya hii inaakisi sifa za kisanii ambazo hazipatikani katika riwaya nyingine zinazobainika katika fasihi ya Kiswahili. Usanii huo unaweza kutokeza kwenye viwango tofautitofauti kama: usimulizi, mitindo ya uashiriaji, matumizi ya lugha, usawiri wa wahusika, matumizi ya mtazamo na kadhalika. Riwaya mpya pia inaonyesha sifa za kimtindo na kimuundo ambazo zinakiuka sifa zinazohusishwa na riwaya ya jadi. Baadhi ya waandishi maarufu wa Tanzania wanaotumia utatatibu huu wa usasabaadaye katika uandishi wao ni: Said Ahmed Mohamed aliyetunga *Babu Alipofufuka* (2001), (2005), *Dunia Yao* (2006) na *Nyuso za Mwanamke* (2010); Emmanuel Mbogo, *Vipuli vya Figo* (1996); William Mkufya, *Ziraili na Zirani* (1999) na Seith Chachage, *Makuadi wa Soko Huria* (2002).

Mitindo ya kimajaribio inabainisha wazi juhudi za mwanzo za kuitoa fasihi andishi ya Tanzania nje ya mipaka ya kitaifa na kuitafutia nafasi na mahali pake kimataifa. Juhudi hizi ziliipa fasihi hii upekee na utambulisho kwenye ramani ya kimataifa.

3.5 Athari za Utandawazi na Tafsiri katika Fasihi

Tafsiri za fasihi andishi za kigeni zilianza kujitokeza katika fasihi ya Kiswahili miaka ya 1970 hadi 1980 lakini zikafifia kuanzia miaka ya 1990. Baadhi ya kazi za fasihi ya Kiafrika zilizoandikwa katika lugha ya Kiingereza zilizotafsiriwa katika lugha ya Kiswahili ni zile zilizoandikwa na *Chinua Achebe*, *Ngugi Wa Thiong'o*, *Sembene Ousmane*, *Wole Soyinka*, *Camara Laye*, *Mongo Beti*, *Peter Abrams* na *Okot p'Bitek*.

Lugha ya Kiswahili pia ina hazina kubwa ya tafsiri za kazi za fasihi zilizotungwa Ulaya na Marekani na waandishi kama vile: *William Shakespeare*, *Moliere*, *Conrad*, *George Orwell* na *Alex Huxley*. Kutoka Urusi kuna tafsiri za waandishi kama vile: *Pushkin*, *Leo Tolstoy*, *Maxim Gorky* na *Nicholai Gogol*. Hata hivyo kuna, haja ya kutafsiri kazi za fasihi kutoka Asia kwa mfano zile zilizoandikwa na waandishi mashuhuri kama vile: *Rabindranath Tagore*, *R K Narayan*, *Vikram Seth*, *Raja Rao*, *Bhati Mukherjee* na *Kirani Desai* (India); *Lien Chao* na *Ha Jin* (China) na kutoka Marekani Kusini kwa mfano zile zilizoandikwa na waandishi kama vile: *Octavia Paz*, *Juan Rulfo* na *Carlos Fauntes* (Mexico); *Jorge Luis Borges* (Argentina); *Alejo Carpentier* (Cuba); *Pablo Neruda* (Chile); *Garbriel Garcia Marquez* (Columbia); *Paulo Coelho* (Brasil) na *Giannina Brasch*

(Puerto Rico).

Athari za utandawazi zinajitokeza katika kazi za fasihi zilizotungwa kuanzia miaka ya 2000 na kwendelea nchini Tanzania. Baadhi ya sifa zinazotambulisha kazi hizi ni: matumizi ya wahusika jumui na wahusika picha, matumizi ya uhali-siamazingaombwe na mitindo ya usasabaadaye, mwingiliano matini, uajinabishaji, usimulizi wa kipolifoni, mvutogubi na ufabulishaji. Baadhi ya

waandishi maarufu wanaotumia mitindo hii ni S. A. Mohamed: *Babu Alipofufuka* (2006) na *Dunia Yao* (2007), W Mkufya: *Ziraili na Zirani* (1999) na S. Chachage *Makuadi wa Soko Huria*.

Changamoto za Ukuaji wa Fasihi 4.0 Andishi nchini Tanzania

Baadhi ya mashirika ya uchapishaji hayako tayari kuchapisha vitabu vya waandishi chipukizi. Jambo hili huwavunja nyoyo waandishi wa Kiswahili ambao wangependa kujiendeleza kitaaluma kupitia uandishi wa vitabu vya riwaya, tamthiliya, ushairi, hadithi fupi na fasihi ya watoto. Suala hili ni la kusikitisha kwani imedaiwa kuwa baadhi ya mashirika ya uchapishaji huchapisha majina ya waandishi na wala sio uzito na ufaafu wa kazi yenyewe.

Ukosefu wa soko ni tatizo lingine linalowakabili waandishi wa vitabu vya Kiswahili nchini Tanzania. Iwapo mwandishi atachapisha kazi yake na kazi hiyo haina nafasi katika mfumo wa elimu hasa shule za msingi na sekondari, huenda asipate mauzo mengi. Hili ni kwa sababu mfumo wa elimu nchini Tanzania umeibua utamaduni wa kusoma kwa minajili ya kufaulu mitihani huku dhima nyingine za kusoma zikiwekwa pembeni.

Uandishi wa vitabu vya Kiswahili mara nyingi huamuliwa na mahitaji ya shule. Wakati mwingine mashirika ya uchapishaji husita kuchapisha kazi ambazo haziwezi kuingizwa katika mfumo wa elimu kama kitabu cha kiada au ziada. Hii ni kwa sababu, soko kubwa la wachapishaji wengi ni shule na vyuo.

Katika uandishi wa vitabu suala la utafiti ni muhimu na la lazima. Baadhi ya waandishi wa Kiswahili hawajamakinika katika mbinu za utafiti. Isitoshe,

ukosefu wa marejeo muhimu ni tatizo kubwa kwa waandishi wa Kiswahili. Baadhi ya dhana za kimsingi za kiisimu na kifasihi zinazofundishwa katika mfumo wa elimu, zinahitaji kutafitiwa kwa kina. Aidha, baadhi ya marejeo hayapatikani kwa urahisi na yakipatikana huwa ghali mno kwa mwandishi anayeanza kazi hii ya uandishi.

Ukosefu wa vifaa vya kisasa vya uandishi kama vile kompyuta. Vifaa hivi kama vile kompyuta ni ghali mno ingawa ni muhimu sana katika taaluma ya uandishi. Wachapishaji wengi hawakubali miswaada ambayo haijapigwa chapa.

Waandishi wengi hasa wa vitabu vya sanaa hulazimisha maudhui. Kuna baadhi ya waandishi wanaotaka kuandika kila utanzu yaani thamthiliya, riwaya, ushairi, hadithi fupi, vitabu vya watoto na vinginevyo jambo ambao haliwezekani kwa waandishi chipukizi.

Athari za utandawazi na utegemezi wa nyenzo nyingine za burudani kama vile filamu na muziki zimezua ushindani mkubwa unaotishia kuangamiza usomaji wa vitabu vya fasihi. Katika muktadha wa utandawazi, sehemu ya jamii inayosoma vitabu ni ile inayohusika pia katika ajira maofisini. Hadhira hii inapotoka kazini hujiburudisha ili kutoa uchovu. Njia inayotegemewa sawa kujiburudisha ni interneti na runimnga; njia hizi zinaathiri pakubwa usomaji vitabu. Ni dhahiri kuwa usomaji wa vitabu umebaki sehemu ya masomo vyuoni.

5.0 Mustakabali wa Fasihi Andishi nchini Tanzania

Fasihi andishi ya Kiswahili nchini Tanzania ina mustakabali bora. Hii ni kwa sababu mataifa mengi ulimwenguni yanategemea kazi za fasihi zinazotungwa Tanzania. Vyuo Vikuu Afrika, Ulaya na Urusi, Asia na Marekani hutegemea kazi za fasihi zilizotungwa Tanzania ili kuzifanyia utafiti. Kuna

haja ya kuhimiza uandishi wa kazi mpya za fasihi ili kuendeleza fasihi ya Kiswahili ya Tanzania. Kuna haja ya kuimarisha utafiti na kutoa mafunzo kwa waandishi chipukizi ili kufikia lengo la kukidhi uhitaji wa kimataifa.

6.0 Hitimisho

Makala haya yamechunguza maendeleo, changamoto na mustakabali wa fasihi andishi nchini Tanzania ndani ya kipindi cha miongo mitano baada ya uhuru. Mikondo mikuu mitano inayobainika kwenye fasihi andishi ya Tanzania imejadiliwa kwa kina.

Mambo mawili yanaweza kuhitimishwa kutokana na mjadala huu. Jambo la kwanza ni kuwa ukuaji

wa fasihi andishi nchini Tanzania ndani ya kipindi cha miaka hamsini ya uhuru umekuwa wa kasi. Hali hii inaweza kutuongoza kufikia hitimisho la pili kuwa mustakabali wa fasihi andishi ya Tanzania utaendelea kuwa bora. Ni dhahiri kuwa tulichonacho hakitoshi kuna haja ya kukiimarisha na kukiboresha ili kukidhi mahitaji ya kimataifa.

Marejeleo

- Bertoncini, E. na Wenzie (2008) *Outline of Swahili Literature* 2nd ed. Leiden: E. J Brill.
- Childs, P. na Fowler (2006) *The Routledge Dictionary of Literary Terms*. London: Routledge.
- Cohan, S na Shires, L (1988) *Telling Stories: A Theoretical Analysis of Narrative Fiction*. London: Routledge.
- Fowler, R. (1996) *Linguistic Criticism*. 2nd edition. Oxford: Oxford University Press.
- Frye, N. (1990) *Anatomy of Criticism: Four Essays*. London: Penguin Books.
- Kezilahabi, E. (1976) *Ushairi wa Shabaan Robert*. Nairobi: Kenya Literature Bureau.
- Mlacha S. A. na Madumulla, J. S. (1991) *Riwaya ya Kiswahili*. Dar-es-Salaam: Dar-es-Salaam University Press.
- Mohamed, S. A. (1995) *Kunga za Nathari*. Nairobi: East African Educational Publishers.
- Msokile, M. (1992) *Misingi ya Hadithi Fupi*. Dar-es-Salaam University Press.
- Wafula, R. M na Njogu, K (2007) *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.
- Wamitila, K. W. (2002) *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele Vyake*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- (2003) *Kamusi ya Fasihi: Istilahi na Nadharia*. Nairobi: Focus Publishers.
- (2008) *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers.